# Ujenzi wa Maana katika Sitiari na Tashibiha za Kiswahili

George J. Kitundu & Pendo S. Malangwa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Ikisiri**

Kwa muda mrefu, tamathali za semi zimekuwa zikichunguzwa na kushughulikiwa zaidi katika uwanja wa fasihi kuliko kwenye isimu. Hali hii imewasababishia watu wengi kuwa na dhana kwamba kipengele hiki ni cha kifasihi tu. Kuna ushahidi kwamba zipo tafiti zilizochunguza vipengele hivi katika nyuga za lugha na isimu. Hata hivyo, kuna mitazamo tofauti, hususani katika namna maana za tamathali za semi zinavyojengwa. Mathalani, baadhi ya wanazuoni wanaona kuwa vipengele vya sitiari na tashibiha vina namna moja ya ujenzi wa maana ilhali wengine wakiamini kuwa vipengele hivi vinatofautiana. Makala hii, kwa kujikita katika uwanja wa semantiki, inadhihirisha kwamba kuna namna maalumu inayotawala ujenzi wa maana katika vipengele vya sitiari na tashibiha. Kila kipengele kina namna yake tofauti ambayo huhusisha mwingiliano wa elementi mbalimbali. Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka katika matini za vitabu na magazeti na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa mwingiliano.

## 1.0 Utangulizi

Sitiari na tashibiha ni dhana ambazo zina namna yake ya ujenzi wa maana kisemantiki. Wataalamu mbalimbali wameeleza namna tamathali hizi zinavyoweza kujenga maana kutokana na mpangilio fulani wa maneno au elementi. Mathalani, Ndimele (1997) anadai kuwa sitiari ni kama tashibiha kwa sababu zote zinalinganisha vitu au matukio mawili na zinahusisha sehemu kuu tatu ambazo ni mada, kibebeo na sifabia. Maelezo ya Ndimele (1997) yanaonesha kuwa tamathali hizi zina namna moja ya ujenzi wa maana inayohusisha elementi tatu, yaani mada, kibebeo na sifabia. Naye Ullmann (1967) anaeleza kuwa muundo wa sitiari unahusisha elementi tatu, yaani mada, kibebeo na sifabia. Kwa hiyo, ili uweze kujenga maana katika sitiari ni lazima uwe na elementi hizo tatu. Fishelov (2007) naye anasema kuwa kisemantiki, tashibiha zinahusisha sehemu tatu, yaani mada, kibebeo na sifabia. Sehemu hizo zinahusiana kwa namna fulani kisemantiki. Maelezo ya Fishelov (2007) yanaonesha kuwa tashibiha zinahusisha elementi tatu katika ujenzi wa maana ambazo ni sawa na zile zinazotajwa na Ullmann (1967) katika sitiari na Ndimele (1997) katika sitiari na tashibiha.

Tofauti na maelezo ya baadhi ya wataalamu tuliowajadili kuhusu elementi zinazohusika katika ujenzi wa maana kwenye tashibiha, Hanks (2012) anaeleza kuwa tashibiha zinahusisha elementi tano ambazo ni mada, tukio, sifa, kilinganishi

pamoja na kibebeo. Katika elementi hizo, Hanks (2012) anaona kuwa mada, kibebeo, sifabia na tukio ni za lazima huku kilinganishi ikiwa siyo elementi ya lazima.

Kwa upande wao Niculae na Mizil (2014) wanakubaliana na mawazo ya Hanks (2012) kuwa ujenzi wa maana katika tashibiha unahusisha elementi hizo tano. Wanaeleza zaidi kuwa katika miaka ya karibuni tashibiha zimekuwa zikichunguzwa sana na zinahitaji kuchunguzwa tofauti na sitiari kwa sababu zina kanuni za msingi ambazo ni tofauti na za sitiari. Kauli ya wataalamu hao inaonesha kuwa tashibiha zina kanuni za msingi ambazo ni tofauti na kanuni za sitiari katika namna tamathali hizi zinavyojengwa. Ndiyo maana wataalamu hawa wanaona si sahihi kusema sitiari ni sawa na tashibiha.

Kwa ujumla, maelezo ya baadhi ya wataalamu kama Ndimele (1997) na Fishelov (2007) yanaonesha kuwa sitiari na tashibiha zina namna inayofanana ya ujenzi wa maana huku wengine kama Hanks (2012) na Niculae na Mizil (2014) wanaonesha kuwa kuna namna tofauti. Jambo hili bado linazua mkanganyiko hivyo kuna haja ya kutafiti zaidi tamathali hizi kwa kutumia lugha mahususi ili kuona kama kuna namna moja ya ujenzi wa maana au tofauti. Kwa hali hiyo, makala hii inachunguza ujenzi wa maana katika sitiari na tashibiha za Kiswahili. Katika uchunguzi huo, kwanza tutajadili dhana ya sitiari na tashibiha kisha kufuatiwa na vipengele vya muundo wa maana, mkabala wa utafiti huu pamoja na mbinu za utafiti. Vilevile, tutajadili ujenzi wa maana katika sitiari na tashibiha sambamba na kulinganisha ujenzi huo wa maana. Kipengele cha mwisho katika makala hii ni hitimisho la jumla.

## 2.0 Dhana za Sitiari na Tashibiha

Sitiari ni tamathali ya semi inayolinganisha vitu viwili vyenye uhusiano fulani kisemantiki. Ulinganishi huo unahusisha mada pamoja na kibebeo (taz. Richards, 1965; Ullmann, 1967; Lakoff na Johnson, 1980; Ndimele, 1997; Stern, 2000; Cruse, 2006 na Fadaee, 2011). Katika ulinganishaji huo kuna uhamishaji wa maana unaojitokeza kutoka kwenye kibebeo kwenda katika mada, hasa kutokana na kuwapo kwa uhusiano fulani wa kisemantiki katika elementi hizo. Akifafanua zaidi kuhusu uhamishaji huo wa maana katika sitiari, Ullmann (1967) anaeleza kuwa kuna uhamishaji wa maana wa aina nne. Kwanza, uhamishaji wa maana unaomhusu binadamu na viungo vyake vya mwili pamoja na vitu visivyo hai. Katika uhamishaji huu, viungo vya mwili wa binadamu huweza kufananishwa na vitu vingine. Mathalani, *mguu wa meza* na *mkono wa saa* ambapo viungo vya mwili wa binadamu kama mkono na mguu vinalinganishwa na vitu mbalimbali katika mazingira, kama vile meza na saa. Pili, kuna uhamishaji wa maana unaohusu tabia mbalimbali za wanyama kuhamishiwa kwa binadamu. Katika aina hii, jamii mbalimbali za wanyama ambao tabia zao zinashabihiana kwa namna

fulani na za binadamu, huhamishiwa kwa binadamu. Mathalani, sitiari *Juma ni simba* ni moja ya mifano katika kundi hili ambapo tabia za mnyama simba zinahamishiwa kwa binadamu, yaani Juma. Aina ya tatu ya uhamishaji wa maana ni ile inayohusisha vitu halisi kwenda dhahania na kinyume chake. Mathalani, sitiari kama *maisha ni moshi, maisha ni mlima* ni baadhi ya mifano katika kundi hili. Uhamishaji wa aina ya nne ni ule unaohusu milango ya fahamu. Kwa mfano, *sauti tamu, sauti baridi* na *pendo tamu* ni baadhi ya mifano katika kundi hili.

Kwa upande mwingine, tashibiha ni tamathali ya semi inayolinganisha vitu viwili kwa kutumia kihusishi *kama* au *mithili ya.* Vitu au dhana zinazolinganishwa huwa na mfanano fulani kisemantiki. Kufanana huko kwa vitu viwili ndiko kunakotoa mwanya kwa msikilizaji au msomaji kujenga uhusiano wa vitu hivyo (Ndimele, 1997; Cruse, 2006; Massamba, 2009; Fadaee, 2011 na Hussain, 2014). Kulingana na namna ulinganishi unavyofanyika, tashibiha zinaweza kuwekwa katika makundi mawili ambayo ni tashibiha halisi na zisizo halisi (Cruse, 2006 na Fadaee, 2011).


Tashibiha halisi ni zile ambazo hutaja sifa inayolinganishwa moja kwa moja. Tashibiha hizi haziachi maswali kwa wasikilizaji juu ya fasili ya tamathali hiyo kwa sababu sifa inayolinganishwa inatajwa wazi. Mathalani, *Meno yake **yaling'aa** kama chuma katika mwanga, Mwanamke mmoja **mnene** kama pipa, alimwita* na *Aliziona nywele za kipilipili za Musa **ngumu** kama katani.* Katika mifano hiyo, sifa inayolinganishwa kati ya mada na kibebeo, yaani sifa za kung'aa, unene na ugumu (zimebainishwa kwa wino koza) zimetajwa wazi. Kutajwa huko wazi kunaifanya tamathali husika kuwa wazi kimaana. Kundi lingine la tashibiha ni zile zisizo halisi. Tashibiha hizi hazibainishi sifa inayolinganishwa kati ya mada na kibebeo. Mathalani, *Meno yake yalikuwa kama chuma.* Katika tashibiha hiyo, sifa inayolinganishwa kati ya mada na kibebeo haitajwi wazi. Kutotajwa wazi kwa sifa linganishwa kunaacha maswali kwa msikilizaji kuwa ni sifa ipi jumuishi inayozungumziwa kati ya meno na chuma. Je, ni sifa ya *ugumu*, *kung'aa* au *rangi*? Katika sehemu inayofuata tunajadili muundo wa maana katika sitiari na tashibiha.

## 3.0 Muundo wa Maana katika Sitiari na Tashibiha

Dhana ya muundo wa maana katika sitiari na tashibiha inarejelea elementi mbalimbali zinazohusika katika ujenzi wa maana. Katika sitiari, muundo wa maana unahusisha elementi tatu ambazo ni mada, kibebeo na sifabia. Elementi hizo ndizo zinazoipa sitiari inayohusika muundo na maana yake (taz. Black, 1962; Richards, 1965; Ullmann, 1967; Leech, 1969; Ndimele, 1997; Holme, 2004; Cruse, 2006; Geeraerts, 2009). Mada inafafanuliwa kuwa ni kile kitu kinachozungumziwa katika usemi. Kibebeo ni kitu kinacholinganishwa na mada, ambacho kwa mujibu wa Griffith (2006), ndicho kinachobeba maana ya kitamathali. Sifabia ni sifa jumuishi za mada na kibebeo. Katika kufafanua zaidi namna maana zinavyojengwa

kwenye sitiari, Hester (1967), Stacy (1977) na Trick na Kanzi (1986) wanadai kuwa ili kuwe na maana za kisitiari, ni lazima kuwe na uhusiano chanya kati ya mada na kibebeo. Japo uhusiano huu si wa moja kwa moja lakini ni dhahiri maneno yanayotumika katika kuunda sitiari huwa na uhusiano chanya. Ufafanuzi zaidi wa namna elementi hizo zinavyojenga maana katika sitiari unaoneshwa katika Kielelezo Na. 1.

**Kielelezo Na. 1: Uhusiano wa Elementi Zinazojitokeza katika Muundo wa Maana kwenye Sitiari**




**Chanzo:** Ayoob (2007) na kimeboreshwa na Kitundu (2018)

Kielelezo Na. 1 kinaonesha kwamba kuna elementi mbili zenye kuhusiana kwa namna fulani katika kujenga maana kwenye sitiari ambazo ni mada na kibebeo. Kutokana na mwingiliano wa elementi za mada na kibebeo tunapata elementi ya tatu ambayo ni sifabia. Sifabia hizo zinachotwa kutoka katika sifa za mada na kibebeo kutokana na kuwapo kwa uhusiano chanya katika elementi hizo. Kujitokeza kwa sifabia ndiko kunakokamilisha ujenzi wa maana katika sitiari husika. Kwa mantiki hiyo, muundo wa maana katika sitiari unahusisha elementi za mada, kibebeo na sifabia.


Tashibiha kwa upande wake nazo zina namna fulani ya ujenzi wa maana inayotokana na kuwapo kwa mwingiliano na mpangilio maalumu wa elementi fulani. Hivyo, si kila mpangilio fulani wa maneno unaweza kuibua maana katika tashibiha (Cruse, 2006). Mathalani, usemi *Your kitchen is very like mine* (Cruse, 2006: 165) katika lugha ya Kiingereza wenye maana ya *Jiko lako ni kama langu* katika lugha ya Kiswahili[1] ni usemi wenye ulinganishi lakini hauna sifa ya kuitwa tashibiha. Maelezo haya yanadokeza kuwa kuna namna inayotawala ujenzi wa maana katika tashibiha jambo ambalo linajadiliwa katika makala haya.

---

[1] Tafsiri hii pamoja na nyingine zitakazofuata ni za waandishi wa makala hii isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo.

Baadhi ya wataalamu wamejaribu kueleza muundo unaotawala ujenzi wa maana katika tashibiha. Mathalani, Ndimele (1997) na Fishelov (2007) wanataja muundo wa tashibiha kuwa unahusisha elementi za mada, kibebeo na sifabia. Maelezo ya wataalamu hawa yanaonesha kuwa kuna namna moja ya ujenzi wa maana katika sitiari na tashibiha ambayo inahusisha elementi hizo tatu. Kwa upande wao Hanks (2012) na Niculae na Mizil (2014) wanaeleza kuwa muundo wa maana katika tashibiha unahusisha elementi tano, yaani *mada*, *tukio*, *sifa*, *kilinganishi* pamoja na *kibebeo*. Katika elementi hizo, *mada* inafafanuliwa kama kitu kinachozungumziwa katika usemi. *Kibebeo* ni kitu kinacholinganishwa na mada katika usemi husika. *Tukio* ni tendo au kitenzi kinachojitokeza katika usemi na ambacho husaidia kudokeza sifabia. *Sifa* huelezea kile ambacho mada na kibebeo zinahusianishwa nacho na *kilinganishi* ni elementi ambayo hutumika kudokeza kuwapo kwa ulinganishi katika usemi. Uhusiano wa elementi hizo unafafanuliwa vizuri katika Kielelezo Na. 2:

**Kielelezo Na. 2: Uhusiano wa Elementi Zinazojenga Muundo wa Maana katika Tashibiha**




**Chanzo:** Ayoob (2007) na kimeboreshwa na Kitundu (2018)

Kielelezo Na. 2 kinaonesha kwamba kuna elementi tano zenye kuhusiana kwa namna fulani katika kujenga maana kwenye tashibiha. Elementi hizo ni mada na kibebeo ambazo kila moja ina sifa zake inayohusishwa nayo. Kati ya sifa hizo za mada na kibebeo, kuna sifa zinazojitokeza pande zote mbili. Sifa hizo ndizo zinazojenga sifabia. Sifabia hizi huweza kutajwa wazi kupitia kivumishi/elementi ya sifa au kudokezwa katika elementi ya tendo. Kwa hiyo, kazi ya elementi ya sifa ni kubainisha sifa inayolinganishwa kati ya mada na kibebeo wakati elementi ya tendo hufanya kazi ya kuweka msingi wa ubainishaji wa sifabia. Elementi nyingine katika ujenzi wa maana ni kilinganishi. Elementi hii hufanya kazi ya kudokeza kuwapo kwa ulinganishi kati ya mada na kibebeo katika usemi. Mwingiliano wa

elementi hizo ndio unaojenga maana katika tashibiha. Kwa mantiki hiyo, muundo wa maana katika tashibiha unahusisha elementi hizo tano.


**4.0 Mkabala wa Uchunguzi wa Sitiari na Tashibiha**

Black (1962) anaeleza kuwa kuna mikabala mitatu inayoweza kutumika kufafanua sitiari na tashibiha. Mikabala hiyo ni ubadala, ulinganishi na mwingiliano. Mkabala wa ubadala unaegemea katika mtazamo kuwa sitiari inatumika badala ya matamshi ya kawaida. Matamshi hayo ya kisitiari yatumikapo, huwa na maana sawa na matamshi ya kawaida. Mathalani, Black (1962:33) anatoa mfano wa "*Richard is a lion"* kuwa unatumika badala ya "*Richard is brave*." Kwa upande mwingine, mkabala wa ulinganishi unaegemea kwenye madai kuwa sitiari ni ulinganishi wa vitu au dhana mbili (Black, 1962). Mkabala huu unaiona sitiari kuwa ni kifupi cha tashibiha. Mathalani, Black (1962:36) anatoa mfano wa *Richard is a lion* katika lugha ya Kiingereza wenye maana *Richard ni simba* katika lugha ya Kiswahili kuwa una maana sawa na *Richard is like a lion* katika lugha ya Kiingereza ambao ni sawa na *Richard ni kama simba* katika lugha ya Kiswahili. Mikabala yote hii miwili, ya ubadala na ulinganishi, si muafaka sana katika kufikia malengo ya makala hii hasa kwa kuwa haielezi ni kwa namna gani maana zinajengwa katika sitiari na tashibiha. Badala yake imejikita kuelezea zaidi matumizi ya sitiari na namna zinavyoweza kuibua tashibiha.

Mkabala wa tatu ni wa mwingiliano ambao unaegemea kwenye madai kuwa maana katika sitiari ni matokeo ya mwingiliano wa dhana mbalimbali za lugha katika harakati za kuuelezea ulimwengu. Dhana hizo ni mada na kibebeo (Black, 1962). Kulingana na mkabala huu, maana katika sitiari ni matokeo ya mwingiliano wa dhana hizo mbili. Mwingiliano wa dhana hizo ndio husababisha kuwapo kwa uhamishaji wa maana na hatimaye kupata maana ya kitamathali. Mkabala huu pia unazungumzia sifa za pamoja za dhana hizo mbili kama msingi wa uibuzi wa maana katika sitiari, yaani sifabia. Sifabia hizo huibuliwa baada ya kuwapo kwa mwingiliano wa mada na kibebeo. Kwa kifupi, mkabala huu unasisitiza kuwa maana za kisitiari ni matokeo ya mwingiliano wa elementi mbalimbali kama vile mada, kibebeo na sifabia. Kila elementi ina umuhimu wake katika ujenzi wa maana (Holme, 2004).

Katika kufafanua zaidi namna mkabala huu unavyofanya kazi, Ayoob (2007) anatumia Kielelezo (taz. Kielelezo namba 3 hapa chini) kubainisha namna elementi za mada na kibebeo zinavyoingiliana na kupata sifabia ambazo ndizo zinazojenga maana mpya ya mada. Anatumia mfano wa *John is a wolf* katika lugha ya Kiingereza wenye maana ya *John ni mbwamwitu* katika lugha ya Kiswahili kwenye ufafanuzi wake kama Kielelezo Na. 3 kinavyoonesha:

**Kielelezo Na. 3: Mwingiliano wa Elementi za Mada, Kibebeo na Sifabia katika Ujenzi wa Maana**




**Chanzo:** Ayoob (2007) na kimeboreshwa na Kitundu (2018)

Kielelezo Na. 3 kinaonesha kuwa kuna sifa zinazohusishwa na mada pamoja na kibebeo. Kati ya sifa hizo, zipo zinazojitokeza katika pande zote mbili. Kujitokeza kwa sifa hizo kunajenga elementi ya tatu, yaani sifabia. Sifabia hizo zinachotwa kutoka katika sifa za mada pamoja na kibebeo. Kuibuka kwa sifabia kunakamilisha ujenzi wa maana katika sitiari hiyo. Kwa hiyo, maana katika sitiari hiyo ni matokeo ya mwingiliano wa elementi tatu yaani mada, kibebeo na sifabia kama Kielelezo Na. 3 kinavyoonesha. Katika makala hii mkabala huu umetumika kuonesha namna elementi mbalimbali zinavyoingiliana katika kujenga maana za sitiari na tashibiha.

## 5.0 Mbinu za Utafiti

Data iliyotumika katika makala haya imekusanywa kutoka katika matini sita ambazo zilitokana na makundi mawili, vitabu na magazeti. Matini hizo ni vitabu vya *Wasakatonge* (Khatib, 2002), *Watoto wa Maman'tilie* (Mbogo, 2008) na *Kilio Chetu* (Medical Aid Foundation, 1995). Vitabu hivi viliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi ambapo kulikuwa na matabaka matatu ya tanzu za fasihi andishi. Matabaka hayo ni pamoja na ushairi, riwaya na tamthiliya. Kutoka kila tabaka kiliteuliwa kitabu kimoja kinasibu ili kuwakilisha vitabu vingine. Kwa upande wa magazeti yaliyoteuliwa ni pamoja na *Majira* linalochapishwa na *Business Printers Limited*, *Mwananchi* linalochapishwa na *Mwananchi Communication Limited*, na *Mtanzania* linalopigwa chapa na *New Habari* (2006) *Limited* ambayo hutolewa kila siku. Magazeti yaliyotumiwa ni yale yaliyochapishwa kwa lugha ya Kiswahili ya tarehe 21/1/2017. Ili kupata data

sahihi kutoka katika matini hizo, mbinu ya uchambuzi wa matini ndiyo iliyotumika katika ukusanyaji wa data (Kothari, 2009).

Uchambuzi wa tamathali katika matini hizo uliongozwa na vigezo mbalimbali. Baadhi ya vigezo hivyo ni pamoja na kutazama muundo wa maana katika tamathali hizo ambao katika sitiari unahusisha mada, kibebeo na sifabia wakati katika tashibiha unahusisha elementi za mada, kibebeo, kilinganishi, sifa na tendo. Kigezo kingine kilichotumika katika kubainisha tamathali hizo ni kuangalia uhusiano wa mada na kibebeo katika maeneo tofauti kisemantiki. Katika tamathali hizo, uhamishaji wa maana huwapo kama mada na kibebeo zitakuwa katika makundi mawili tofauti kisemantiki. Mathalani, katika mfano wa *Juma ni simba* au *Juma ni kama simba*, *Juma* na *simba* ni viumbe tofauti, hivyo kudokeza kuwapo kwa sitiari au tashibiha. Pamoja na vigezo hivyo, mbinu nyingine iliyotumika katika kubainisha tashibiha na kuzitofautisha na sitiari ni kwa kuangalia matumizi ya maneno ambayo ni vifananishi (Griffiths, 2006). Vifananishi hivyo katika lugha ya Kiswahili ni pamoja na "kama" au "mithili ya". Uchambuzi wa data ya utafiti huu ulifanyika kwa kutumia mbinu linganishi (Ragin, 1987), hasa kwa kuwa lengo la makala hii ni kulinganisha pia ujenzi wa maana katika tamathali hizo.

## 6.0 Ujenzi wa Maana katika Sitiari na Tashibiha za Kiswahili

Dhana ya ujenzi wa maaana katika makala hii tumeijadili kama namna elementi mbalimbali zinavyoingiliana ili kujenga maana katika tamathali inayohusika. Katika sehemu inayofuata tutafafanua namna maana zinavyojengwa katika sitiari na tashibiha.

### 6.1 Ujenzi wa Maana katika Sitiari

Maana katika sitiari zinajengwa kutokana na kuwapo kwa mwingiliano wa elementi kadhaa. Katika sehemu hii, sitiari mbalimbali zimechambuliwa kwa kutumia Mkabala wa Mwingiliano ili kuona namna maana zake zinavyojengwa. Katika uchambuzi huu wa data, alama "M" imetumika kurejelea mada, "K" inarejelea kibebeo na "SB" inarejelea sifabia. Katika uchunguzi huu, uhusiano wa elementi zinazohusika katika ujenzi wa maana umeoneshwa kwa kutumia kielelezo kilichoboreshwa na Kitundu (2018). Kulingana na data iliyokusanywa[2], uchambuzi wa ujenzi wa maana katika sitiari unaonekana kama ifuatavyo:


1. Mwili ulikuwa tanuri la moto (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 46)
   M: mwili
   K: tanuri la moto
   SB: joto

Katika sitiari hiyo, kuna mwingiliano wa elementi tatu zinazojenga maana. Elementi hizo ni mada ambayo ni mwili, kibebeo ambacho ni tanuri la moto na

[2] Data hizi zilitumiwa pia katika utafiti wa Kitundu (2018).

sifabia ambayo ni joto. Ufafanuzi zaidi kuhusu elementi hizo katika ujenzi wa maana unaoneshwa vizuri kupitia Kielelezo Na. 4 kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na. 4: Sitiari ya Mwili na Tanuri la Moto**





Katika Kielelezo Na. 4 kuna sifa zinazohusishwa na mwili (mada) na tanuri la moto (kibebeo). Kati ya sifa hizo, ipo inayojitokeza katika pande zote mbili. Sifa hiyo ndiyo inayojenga elementi ya tatu, yaani sifabia. Kuibuka kwa sifabia kunakamilisha ujenzi wa maana katika sitiari hiyo. Katika ujenzi huo wa maana, dhana ya joto la tanuri la moto inahamishiwa katika mwili wa binadamu ambao nao huwa na joto kali wakati fulani. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ujenzi huu wa maana katika sitiari tuangalie mfano ufuatao:

2. Uchoyo ni sumu (Diwani ya *Wasakatonge*, uk. 35)
   M: uchoyo
   K: sumu
   SB: hatari

Katika sitiari hiyo, maana imejengwa kutokana na mwingiliano wa elementi za mada ambayo ni uchoyo, kibebeo ambacho ni sumu na sifabia ambayo ni hatari. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ujenzi wa maana katika sitiari hii, tutazame Kielelezo Na. 5:

**Kielelezo 5: Sitiari ya Uchoyo na Sumu**





**Chanzo:** Data ya Maktabani (2018)

Kielelezo Na. 5 kinaonesha kuwa kuna sifa zinazohusishwa na uchoyo pamoja na sumu. Kati ya sifa hizo, kuna sifa ya hatari inayojitokeza katika elementi zote. Kuwapo kwa sifa hiyo, kunaibua elementi ya tatu, yaani sifabia ambayo ndiyo inayokamilisha ujenzi wa maana katika sitiari hiyo. Mwingiliano na uhusiano wa elementi hizo unasababisha hali ya hatari inayohusishwa na sumu kuhamishiwa katika uchoyo ambao nao ni hatari kwa sababu unaweza kuleta madhara kama ilivyo kwa sumu. Ufafanuzi zaidi kuhusu ujenzi wa maana kwenye sitiari, unatolewa katika mfano unaofuata:

3. Wanasiasa vinyonga. Na waumini vinyonga (Diwani ya *Wasakatonge*, uk. 49)
   M: wanasiasa/waumini
   K: vinyonga
   SB: tabia ya kubadilikabadilika

Ujenzi wa maana katika sitiari hii unatokana na mwingiliano wa elementi za mada, kibebeo na sifabia. Mada ni wanasiasa/waumini. Kibebeo ni kinyonga, mnyama mwenye sifa ya kubadilikabadilika rangi ili kuendana na mazingira aliyomo (TUKI, 2013) na sifabia ni tabia ya kubadilikabadilika au kutokuwa na msimamo inayohusishwa kati ya mada na kibebeo. Kwa muhtasari kuhusu ujenzi wa maana katika sitiari hiyo, tutazame Kielelezo Na. 6:

**Kielelezo Na. 6: Sitiari ya Wanasiasa/waumini na Vinyonga**





**Chanzo:** Kitundu (2018)

Kielelezo Na. 6 kinaonesha kuwa kuna sifa zinazohusishwa na wanasiasa/waumini pamoja na vinyonga. Kati ya sifa hizo, kuna sifa ya kubadilikabadilika inayojitokeza katika pande zote mbili. Kujitokeza kwa sifa hiyo ndiko kunakoibua elementi ya tatu, yaani sifabia. Kuibuka kwa sifabia kunakamilisha ujenzi wa maana katika tamathali hiyo. Katika sitiari hiyo, tabia aliyonayo kinyonga ya kubadilikabadilika rangi katika mazingira mbalimbali inahamishiwa kwa watu wenye tabia ya kubadilika kimsimamo na/au kimatendo. Ufafanuzi zaidi kuhusu ujenzi wa maana katika sitiari unaendelea kutolewa katika data inayofuata:

4. Sheria ni pumzi (Gazeti la *Mtanzania*, uk. 13)
   M: sheria
   K: pumzi
   SB: umuhimu/uthamani wake

Ujenzi wa maana katika sitiari hii unatokana na mwingiliano wa elementi za mada ambayo ni sheria, kibebeo ambacho ni pumzi na sifabia ambayo ni uthamani au umuhimu. Kielelezo Na. 7 kinafafanua zaidi ujenzi wa maana katika sitiari hiyo.

**Kielelezo Na. 7: Sitiari ya Sheria na Pumzi**





**Chanzo:** Kitundu (2018)

Kielelezo Na. 7 kinaonesha kuwa kuna sifa zinazojitokeza kati ya sheria (mada) na pumzi (kibebeo). Kati yake kuna sifa za uthamani na umuhimu zinazojitokeza katika pande zote mbili. Kujitokeza kwa sifa hizo kunaibua elementi ya sifabia. Kujitokeza kwa sifabia kunakamilisha ujenzi wa maana katika sitiari hiyo. Kutokana na mwingiliano na uhusiano wa elementi hizo, umuhimu wa pumzi kwa kiumbe hai unahamishiwa katika sheria ambayo nayo ina umuhimu wake katika jamii. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ujenzi wa maana katika sitiari tutazame data inayofuata:

5. Vijana ni nguzo (Gazeti la *Majira*, uk. 5)
   M: vijana
   K: nguzo
   SB: umuhimu

Sitiari hii imejengwa kutokana na mwingiliano wa elementi tatu za mada, kibebeo na sifabia. Mada ni vijana, kibebeo ni nguzo na sifabia ni umuhimu unaojitokeza kwa vijana na nguzo. Ili kuweza kufahamu zaidi namna maana ilivyojengwa katika sitiari hiyo, tutazame Kielelezo Na. 8:

**Kielelezo Na. 8: Sitiari ya Vijana na Nguzo**




**Chanzo:** Kitundu (2018)

Kielelezo Na. 8 kinaonesha kuwa kuna sifa zinazohusishwa na mada (vijana) pamoja na kibebeo (nguzo). Kati ya sifa hizo, kuna sifa ya umuhimu inayojitokeza katika pande zote mbili. Kujitokeza kwa sifa hiyo kunaibua elementi ya sifabia. Kuibuka kwa sifabia kunakamilisha ujenzi wa maana katika tamathali hiyo. Katika sitiari hiyo, umuhimu wa nguzo katika kushikilia kitu kingine unahamishiwa kwa vijana ambao nao ni muhimu katika jamii.

Kwa ujumla, katika uchambuzi huo wa data tunaona kuwa ujenzi wa maana katika sitiari unahusisha elementi za mada, kibebeo na sifabia. Mwingiliano wa elementi hizo ndio unaojenga maana katika sitiari. Katika ujenzi huo wa maana, mada na kibebeo vina uhusiano fulani kisemantiki. Uhusiano huo ni ule wa kutoka katika kategoria moja ya nomino. Hii ina maana kuwa, mada na kibebeo katika lugha ya Kiswahili vinajengwa na nomino mbili tofauti. Nomino hizo pamoja na kuwa ni tofauti lakini zina sifa fulani zinazofanana. Kuwapo kwa sifa zinazofanana ndiko kunakotoa mwanya wa kujitokeza kwa sifabia. Kujitokeza kwa sifabia kunakamilisha ujenzi wa maana katika sitiari husika. Baada ya kuangalia ujenzi wa maana katika sitiari, sehemu inayofuata inajikita kuchunga ujenzi wa maana katika tashibiha.

## 6.2 Ujenzi wa Maana katika Tashibiha

Tashibiha kama ilivyo kwa sitiari katika lugha ya Kiswahili, nazo zina namna yake ya ujenzi wa maana inayohusisha mwingiliano wa elementi mbalimbali. Katika sehemu hii, tashibiha mbalimbali zimechambuliwa kwa kutumia Mkabala wa Mwingiliano ili kuona namna maana zinavyojengwa. Katika uchambuzi huo wa data, alama mbalimbali zimetumika. Alama hizo ni pamoja na "M" inayotumika kurejelea mada, "K" inarejelea kibebeo, "S" inarejelea sifa (kwa maana ya kivumishi), "KL" inarejelea kilinganishi na "T" inarejelea tendo/kitenzi. Katika


uchunguzi huu, uhusiano wa elementi zinazohusika katika ujenzi wa maana umeoneshwa kwa kutumia Kielelezo kilichoboreshwa na Kitundu (2018). Kulingana na data iliyokusanywa, uchambuzi wa ujenzi wa maana katika tashibiha unaonekana kama ifuatavyo:

1. Shoga mbona unakuwa mgumu kama mpingo? (Tamthiliya ya *Kilio Chetu*, uk.. 6)

    M: shoga
    T: unakuwa
    S: mgumu
    KL: kama
    K: mpingo

Katika tashibiha hiyo, maana imejengwa kutokana na mwingiliano wa elementi mbalimbali. Elementi hizo ni pamoja na mada ambayo ni shoga, kibebeo ambacho ni mpingo, tendo ni unakuwa, sifa inayolinganishwa kati ya mada na kibebeo ni ugumu na kilinganishi kinachodokeza kuwapo kwa ulinganishi kati ya mada na kibebeo katika usemi huo ni kama. Ili kuelewa zaidi namna maana inavyojengwa katika tashibiha hii, tutazame Kielelezo Na. 9:

**Kielelezo Na. 9: Tashibiha ya Shoga, Kama, Ugumu, Kuwa na Mpingo**




**Chanzo:** Kitundu (2018)

Kielelezo Na. 9 kinaonesha kuwa kuna sifa zinazohusishwa na shoga (mada) pamoja na mpingo (kibebeo). Kati ya sifa hizo, kuna sifa ya ugumu inajitokeza katika elementi zote. Sifa hiyo imetajwa wazi kupitia kivumushi, yaani elementi ya sifa. Kuwapo kwa sifa hiyo kunadokeza moja kwa moja eneo ambalo mada na kibebeo vinahusianishwa. Katika ujenzi huo wa maana, elementi ya tendo inafanya kazi ya kusaidia kudokeza sifa inayohusishwa wakati kilinganishi kinaashiria kuwapo kwa ulinganishi kati ya mada na kibebeo. Kutokana na mwingiliano huo,


sifa ya ugumu wa rafiki wa kike (shoga) katika kuelewa jambo inalinganishwa na ugumu wa mti wa mpingo. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu ujenzi huo wa maana katika tashibiha, tutazame data ifuatayo:

2. Kurwa aliruka nyuma kama chui (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 24)

M: Kurwa
T: aliruka
S: -
KL: kama
K: chui

Katika tashibiha hiyo, ujenzi wa maana unahusisha elementi za mada ambayo ni Kurwa, kibebeo ambacho ni chui, tendo ni ruka linalofanywa na chui pamoja na Kurwa. Sifa haikutajwa wazi wakati kilinganishi kinachoashiria kuwapo kwa ulinganishi wa mada na kibebeo katika usemi huo ni kama. Ufafanuzi zaidi kuhusu namna elementi hizo zinavyojenga maana kwenye tashibiha hiyo, unatolewa katika Kielelezo Na. 10 kama ifuatavyo:

**Kielelezo Na. 10: Tashibiha ya Kurwa, Kama, Chui na Ruka**




**Chanzo:** Kitundu (2018)


Kielelezo Na. 10 kinaonesha kuwa kuna sifa zinazohusishwa na Kurwa (mada) pamoja na chui (kibebeo). Kati ya sifa hizo, kuna inayojitokeza katika pande zote mbili. Sifa hiyo ni ya kuruka na inadokezwa kupitia elementi ya tendo na si kupitia elementi ya sifa. Kwa hiyo, katika ujenzi wa maana kwenye tashibiha hiyo, sifabia imedokezwa katika elementi ya tendo. Hii ina maana kuwa tendo katika usemi huo linabeba dhima mbili, za kutambulisha tendo katika usemi pamoja na kudokeza sifa inayolinganishwa kati ya mada na kibebeo. Kutokana na mwingiliano wa elementi hizo, Kurwa analinganishwa na chui katika tendo la kuruka. Kwa

ufafanuzi zaidi kuhusu maana zinavyojengwa kwenye tashibiha, tutazame data ifuatayo:

3. "Mwanamke mmoja mnene kama pipa"Alimuita. (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 74)
   M: mwanamke
   S: mnene
   KL: kama
   K: pipa
   T: alimuita

Maana ya tashibiha hii imejengwa kutokana na mwingiliano wa elementi za mada, kibebeo, kilinganishi, sifa na tendo. Mada ni mwanamke mwenye sifa ya unene. Kibebeo ni pipa, chombo chenye sifa ya ukubwa. Tendo ni alimwita. Sifa inayohusishwa kati ya mada na kibebeo ni ya unene na kilinganishi kinachodokeza kuwapo kwa ulinganishaji kati ya elementi za mada na kibebeo katika usemi huo ni kama. Kielelezo Na. 11 kinafafanua zaidi ujenzi wa maana katika tashibiha hiyo:

**Kielelezo Na. 11: Tashibiha ya Mwanamke, Kama, Pipa, Mnene na Ita**





**Chanzo:** Kitundu (2018)

Kielelezo Na. 11 kinaonesha kuwa kuna sifa zinazohusishwa na mwanamke (mada) pamoja na pipa (kibebeo). Kati ya sifa hizo, sifa ya unene inajitokeza katika pande zote mbili. Sifa hii imebainishwa kupitia elementi ya sifa, yaani kivumishi. Elementi nyingine katika kielelezo hicho ni tendo ambalo linaisaidia elementi ya sifa katika ubainishaji wa sifabia. Katika tamathali hiyo, mwanamke analinganishwa na pipa katika sifa ya unene/ukubwa. Ili kupata ufafanuzi zaidi kuhusu ujenzi wa maana katika tashibiha, tutazame data inayofuata:

4. Jina lake lilikuwa refu kama treni ya Kigoma (Gazeti la *Mwananchi*, uk. 21)
   M: Jina
   T: lilikuwa
   S: refu
   KL: kama
   K: treni ya Kigoma

Maana ya tashibiha hii ni matokeo ya mwingiliano wa elementi za mada ambayo ni jina la mtu, kibebeo ambacho ni treni ya Kigoma, tendo ni lilikuwa, sifa ni urefu na kilinganishi kinachodokeza kuwapo kwa ulinganishi wa mada na kibebeo ni kama. Ili kuweza kufahamu zaidi namna elementi hizo zinavyojenga maana kwenye tashibiha hiyo, tutazame Kielelezo Na. 12:

**Kielelezo Na. 12: Tashibiha ya Jina, Treni ya Kigoma, Kama, Refu na Kuwa**




**Chanzo:** Kitundu (2018)


Kielelezo hicho kinaonesha kuwa kuna sifa zinazohusishwa na jina la mtu (mada) na treni ya Kigoma (kibebeo). Kati ya sifa hizo, sifa ya urefu inayojitokeza pande zote mbili. Sifa hii ndiyo inayolinganishwa kati ya mada na kibebeo ikisaidiwa na elementi ya tendo. Katika tashibiha hiyo, urefu wa jina la mtu unalinganishwa na urefu wa treni ya Kigoma. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu namna maana zinavyojengwa katika tashibiha, tutazame data unayofuata:

5. Aliiona miguu ile pekupeku yenye ngozi iliyokatika ikiwa ngumu kama ya mamba (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 14)
   T: aliiona
   M: ngozi ya miguu
   S: ugumu
   KL: kama

K: mamba (ngozi ya mamba)

Maana ya tamathali hii imejengwa kutokana na mwingiliano wa elementi mbalimbali. Elementi hizo ni pamoja na mada ambayo ni ngozi ya miguu, kibebeo ambacho ni mamba, tendo ni aliiona, sifa ni ugumu na kilinganishi kati ya mada na kibebeo ni kama. Kielelezo Na. 13 kinafafanua zaidi ujenzi wa maana katika tashibiha hiyo:

**Kielelezo Na. 13: Tashibiha ya Ngozi ya Miguu, Mamba, Kama, Ngumu na Ona**




Katika kielelezo hicho kuna sifa zinazojitokeza kati ya ngozi ya miguu (mada) pamoja na mamba (kibebeo). Kati ya sifa hizo, sifa ya ugumu inajitokeza katika pande zote mbili. Sifa hiyo inabainishwa na kivumishi huku ikisaidiwa na elementi ya tendo. Kutokana na mwingiliano na uhusiano wa elementi hizo, ugumu wa ngozi ya miguu ya mtu unalinganishwa na ugumu wa ngozi ya mamba. Kwa hiyo, uhusiano wa mada na kibebeo unaonekana kupitia sifa ya ugumu.

Kwa ujumla, kutokana na uchambuzi huo wa data, inaonekana kuwa ujenzi wa maana katika tashibiha unahusisha elementi tano, yaani *mada, kibebeo, kilinganishi, tendo* na *sifa/sifabia.* Katika elementi hizo, ujitokezaji wake unategemea sana aina au namna tashibiha hiyo ilivyojengwa. Katika ujenzi huo wa maana kila elementi ni ya muhimu hata kama haijitokezi dhahiri kama ilivyo kwa baadhi ya tashibiha. Hii ina maana kuwa wakati mwingine katika ujenzi huo wa maana, kuna elementi ambazo hazitajwi wazi katika usemi bali kuwapo kwake hudhihirika kupitia elementi zingine. Mathalani, ikiwa sifa haitajwi wazi kupitia kivumishi basi huweza kudokezwa katika elementi ya tendo au hubainika baada ya kubainishwa kwa sifa za mada na kibebeo (taz. data Na. 2).

Katika elementi hizo tano, uchambuzi wa data unaonesha kuwa mada na kibebeo katika lugha ya Kiswahili vinajengwa na nomino au kirai nomino. Hii ni

tofauti na maelezo yaliyowahi kutolewa na Hanks (2012) kwamba kibebeo kinaweza pia kuwa ni kitenzi au kivumishi. Kwa upande wa elementi ya sifa, kategoria inayohusika ni kivumishi. Hata hivyo, uchambuzi wa data unaonesha kuwa katika lugha ya Kiswahili, iwapo sifa haitajwi wazi (kupitia kivumishi) basi kielezi au kitenzi (kikiwa kipo katika usemi) huweza kudokeza sifa hiyo. Kwa hiyo, katika mazingira fulani ya ujenzi wa maana kwenye tashibiha za Kiswahili tendo hubeba dhima mbili, yaani kusaidia elementi ya sifa katika ubainishaji wa sifabia na pia kudokeza sifabia kati ya mada na kibebeo ikiwa elementi ya sifa haikutajwa wazi katika usemi husika. Kwa hiyo, sifabia katika ujenzi wa maana kwenye tashibiha inaweza kudokezwa na kategoria tatu-kivumishi, kielezi na kitenzi. Elementi ya kilinganishi hufanya kazi ya kudokeza kuwapo kwa ulinganishi wa mada na kibebeo katika usemi husika. Baada ya kufafanua ujenzi wa maana katika sitiari na tashibiha za Kiswahili, kipengele kinachofuata kinajadili ufanano na utofauti uliopo wa ujenzi wa maana katika tamathali hizo.

## 7.0 Ufanano na Utofauti wa Ujenzi wa Maana katika Sitiari na Tashibiha za Kiswahili

Kutokana na uchambuzi wa data uliofanyika, kuna kutofautiana na kufanana kwa sitiari na tashibiha katika ujenzi wa maana. Kutofautiana na kufanana huko kunajadiliwa katika sehemu inayofuata.

### 7.1 Utofauti katika Ujenzi wa Maana

Kulingana na uchambuzi na ufafanuzi wa data uliofanyika katika kipengele cha 6.0, tumebaini kuwa kuna utofauti mkubwa unaojitokeza katika ujenzi wa maana kwenye sitiari na tashibiha za Kiswahili. Tofauti kubwa inayojitokeza katika tamathali hizi iko katika muundo unaotawala ujenzi wa maana, yaani elementi zinazohusika katika ujenzi huo wa maana. Katika sitiari, muundo wa maana unahusisha elementi tatu, yaani *mada, kibebeo* na *sifabia*. Mwingiliano wa elementi hizo ndio unaojenga maana kwenye sitiari husika. Hii ni tofauti katika tashibiha ambayo ina muundo tofauti wa ujenzi wa maana unapoilinganisha na sitiari. Katika tashibiha, muundo wa maana unahusisha elementi tano. Elementi hizo ni *mada, kibebeo, tendo, sifabia* pamoja na *kilinganishi.* Elementi hizi ndizo zinazohusika katika ujenzi wa maana kwenye tashibiha. Mifano katika Jedwali Na. 1 inadhihirisha tofauti hiyo ya muundo wa maana:

**Jedwali 1: Miundo ya Maana katika Sitiari na Tashibiha**

| Sitiari | Tashibiha |
|---|---|
| 1. Ukongwe ni dawa na si simu (Gazeti la *Majira*, uk. 6)<br>M: ukongwe<br>K: dawa<br>SB: umuhimu/uthamani<br>2. Ukongwe ni dawa na si simu (Gazeti la *Majira*, uk. 6)<br>M: ukongwe<br>K: dawa<br>SB: umuhimu/uthamani<br>3. Vijana wamekuwa bendera kufuata upepo (Gazeti la *Mwananchi*, uk. 25)<br>M: vijana<br>K: bendera<br>SB: kutokuwa na msimamo<br>4. Miamba, chui na simba, mbugani wanatamba (Diwani ya *Wasakatonge*, uk. 29)<br>M: viongozi<br>K: chui/simba<br>SB: usaliti/unyanyasaji/unyonyaji<br>5. Jukwaa meingiliwa, wanasiasa Vinyonga, Membari imevamiwa, na waumini vinyonga (Diwani ya *Wasakatonge*, uk. 49)<br>M: Watu (wanasiasa, viongozi wa dini, waumini)<br>K: vinyonga<br>SB: kubadilikabadilika | 6. Leo mtoto kanitolea nje kabisa tena **mkali** pilipili si kitu (Tamthiliya ya *Kilio Chetu*, uk. 19)<br>M: Mtoto (Msichana)<br>T: kanitolea<br>SB: ukali<br>KL: kama<br>K: pilipili<br>7. Aliziona nywele za kipilipili za Musa, ngumu kama katani (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 18)<br>T: aliziona<br>M: nywele za kipilipili<br>SB: ngumu<br>KL: kama<br>K: katani<br>8. Wewe nawe unakuwa nyumanyuma kama koti (Tamthiliya ya *Kilio Chetu*, uk. 5)<br>M: wewe (Mama Suzi)<br>T: unakuwa<br>SB: nyumanyuma<br>KL: kama<br>K: koti<br>9. Kurwa hakupigana bali **aliinama** kama kondoo (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 61)<br>M: Kurwa<br>T: hakupigana<br>SB: inama<br>KL: kama<br>K: kondoo<br>10. Imekuwa ni donda, donda lisilotibika. Lanuka kama ng'onda (Diwani ya *Wasakatonge*, uk. 4)<br>M: donda<br>T: lanuka<br>KL: kama<br>K: ng'onda<br>SB nuka (harufu) |

**Chanzo:** Kitundu (2018)

Data katika Jedwali Na. 1 inaonesha utofauti uliopo katika muundo wa maana kwenye sitiari na tashibiha. Katika safu ya sitiari Na. 1-5 tunaona muundo wa maana ukiwa unahusisha elementi tatu; mada, kibebeo na sifabia wakati katika safu ya tashibiha Na. 6-10 muundo wa maana ukiwa unahusisha elementi tano; mada, kibebeo, tendo, sifa pamoja na kilinganishi.

### 7.2 Ufanano katika Ujenzi wa Maana

Kulingana na uchambuzi na ufafanuzi wa data uliofanyika katika kipengele cha 6.0, tumebaini kuwa, licha ya kuwapo kwa utofauti katika ujenzi wa maana kwenye sitiari na tashibiha za Kiswahili, kuna ufanano fulani unaojitokeza. Ufanano huo upo katika kategoria za maneno zijengazo mada na kibebeo. Katika ujenzi wa maana kwenye sitiari na tashibiha, tumebaini kuwa mada na kibebeo katika tamathali zote zinafanana katika kipengele cha kategoria zitumikazo katika ujenzi huo wa maana. Kulingana na uchambuzi wa data, mada na kibebeo vinatoka katika kategoria moja ya nomino au kirai-nomino; hivyo, zina uhusiano fulani kisemantiki. Kutoka huku katika kategoria moja ya kirai-nomino ndiko kunakotoa mwanya wa kuwapo kwa ulinganishi au uhamishaji wa maana kutoka neno moja kwenda jingine. Ufafanuzi zaidi kuhusu hoja hii unatolewa katika Jedwali Na. 2. Katika Jedwali hilo, alama ya N au KN imewekwa mbele ya elementi ya mada au kibebeo kuashiria kuwa elementi hiyo inajengwa na Nomino au Kirai Nomino.

**Jedwali 2: Kategoria za Maneno Zijengazo Mada na Kibebeo**

| Sitiari | Tashibiha |
|---|---|
| 11. Sheria ni nyenzo (Gazeti la *Mtanzania*, uk. 13)<br>M: sheria-N<br>K: nyenzo-N<br>SB: umuhimu<br>12. Punde dubwana kubwa likaingilia kisiwa kile na kukawa kutafutana (Tamthiliya ya *Kilio Chetu*, uk. 1)<br>M: UKIMWI-N<br>K: dubwana-N<br>SB: hatari, kuenea, kitu cha ajabu<br>13. Mtoto kesha vile mpaka kageuka kizuka (Tamthiliya ya *Kilio Chetu*, uk. 5)<br>M: mtoto-N<br>K: kizuka-N<br>SB: uajabu, enye kutisha<br>14. Usijigeuze popo, huku na huku kutanda (Diwani ya *Wasakatonge*, | 16. Maumivu makali yalisambaa kama cheche (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 46)<br>M: maumivu makali-KN<br>T: yalisambaa<br>KL: kama<br>K: cheche-N<br>SB: enye kasi, kwa haraka<br>17. Mwanamke ni **mrembo** kama chombo chenye ushawishi Diwani ya *Wasakatonge*, uk. 16)<br>M: mwanamke-N<br>T: ni<br>SB: urembo<br>KL: kama<br>K: chombo-N<br>18. Maumivu makali **yalisambaa** kwa kasi kama cheche (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 46) |

| | |
|---|---|
| uk. 27)<br>M: mpenzi-N<br>K: popo-N<br>SB: kutokueleweka/usaliti<br>15. **Ujana** ni chemchem (Gazeti la *Mwannchi*, uk. 25)<br>M: vijana-N<br>K: chemchemi-N<br>SB: chanzo cha kitu (umuhimu) | M: maumivu-N<br>T: yalisambaa<br>KL: kama<br>K: cheche-N<br>SB: kasi<br>19. Vikundi vya ngoma vikachipuka kama uyoga (Gazeti la *Mtanzania*, uk. 12)<br>M: vikundi vya ngoma-KN<br>T: vikachipuka<br>KL: kama<br>K: uyoga-N<br>SB: wingi<br>20. Mate yenye harufu ya gongo **yalitoka** kama cheche za moto (Riwaya ya *Watoto wa Maman'tilie*, uk. 12)<br>M: mate yenye harufu ya gongo-KN<br>T: toka<br>SB: kasi (kutoka kwa kasi)<br>KL: kama<br>K: cheche za moto-KN |

**Chanzo:** Kitundu (2018)

Data kwenye Jedwali Na. 2, hususani Na.11 hadi 20 inaonesha kuwa mada ambazo ni sheria UKIMWI, mtoto, mpenzi, vijana, maumivu, mwanamke, vikundi vya ngoma, mate yenye harufu ya gongo na vibebeo ambavyo ni nyenzo, kizuka, popo, chemchemi, cheche, chombo, uyoga, cheche za moto vyote vinajengwa na kategoria ya nomino au kirai-nomino. Maelezo haya yaliwahi kuelezwa pia na Niculae na Mizil (2014) kuwa mada na kibebeo mara nyingi hubebwa na kirai-nomino. Kwa hiyo, katika ujenzi wa maana kwenye tamathali hizo kuna kufanana katika kipengele cha uhusiano wa mada na kibebeo hasa kwa kuwa elementi zote hizo hutawaliwa na kirai-nomino.

## 8.0 Hitimisho

Makala hii ilikusudia kuchunguza ujenzi wa maana katika sitiari na tashibiha za Kiswahili. Katika uchunguzi huo imebainika kuwa maana katika sitiari zinajengwa kutokana na mwingiliano wa elementi tatu ambazo ni mada, kibebeo na sifabia wakati katika tashibiha maana zinajengwa kutokana na mwingiliano wa elementi tano, mada, kibebeo, sifa/sifabia, kilinganishi pamoja na tendo. Mwingiliano wa elementi hizo ndio unaoibua maana katika tamathali husika. Kila elementi ina umuhimu wake katika ujenzi wa maana kwenye tamathali husika, hivyo hakuna elementi ambayo si ya lazima katika ujenzi wa maana. Vilevile, katika makala hii

imebainika kuwa kuna kufanana na kutofautiana kwa sitiari na tashibiha katika ujenzi wa maana. Tofauti hizo ziko katika muundo unaotawala ujenzi wa maana ambapo katika sitiari elementi tatu ndizo zinazohusika wakati katika tashibiha elementi tano ndizo zinazohusika. Kwa upande wa ufanano, tamathali hizi zinafanana katika kategoria za maneno zijengazo mada na kibebeo, yaani elementi zote hizo zinajengwa na nomino au kirai nomino. Pamoja na maelezo hayo, makala hii inapendekeza pia kufanyika kwa tafiti zaidi za kiisimu katika vipengele vingine vya tamathali za semi ambavyo navyo huenda vina namna yake ya ujenzi wa maana kisemantiki. Tafiti hizo zitaendelea kutoa maarifa mapya ya kitaaluma katika eneo hilo.

## Marejeleo


Ayoob, E. (2007). Black and Davidson on Metaphor, *Macalester Journal of Philosophy*, 16(6): 56-57.

Black, M. (1962). *Models and Metaphors: Studies in Language and Philosophy*. New York: Cornell University Press.

Cruse, A. (2006). *Glossary of Semantics and Pragmatics.* Edinburgh: Edinburgh UP.

Fadaee, E. (2011). Symbols, Metaphor and Simile in Literature*:* A Study of Animal Farm, *Journal of English and Literature*, 2(2):19-27.

Fishelov, D. (2007). Simile Understanding and Semantic Categories, *JLS,* 36:71-78.

Geeraerts, D. (2009). *Theories of Lexical Semantics.* New York: Oxford University Press.

Griffiths, P. (2006). *An Introduction to English and Pragmatic*. Edinburgh: Edinburgh UP.

Hanks, P. (2012). The Roles and Structure of Comparisons, Similes, and Metaphors in Natural Language, *Research Institute for Information and Language Processing,* in www.english.su.se/.../SMF_2012_Patrick. 7/9/2016.

Hester, M, B. (1967). *The Meaning of Poetic Metaphor*. The Hague: Mouton Publishers.

Holme, R. (2004). *Mind, Metaphor and Language Teaching.* New York: Palgrave Macmillan.

Hussain, R. (2014). Metaphors and Simile in Literature, *International Journal of Humanities and Social Science Invension,* 3(9):1-2.

Khatib, M. S. (2002). *Wasakatonge.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Kihore, Y. M. (2004). Masuala ya Kisarufi katika Magazeti ya Mitaani ya Kiswahili Tanzania, *Swahili Forum,* XI: 107-119.

Kitundu, G. J. (2018). Ujenzi wa Maana katika Sitiari na Tashibiha: Uchunguzi Kifani kutoka katika Matini Teule za Kiswahili, Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology: Methods and Techniques*. Jaipur: New Age International (P) Ltd Publishers.

Lakoff, G. & Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live By*. Chicago: Chicago UniversityPress.

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. New York: Long Man Inc.

Massamba, D. P. B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbogo, E. (2008). *Watoto wa Maman'tilie.* Dar es Salaam: Nyambari Nyanginwe Publishers.

Medical Aid Foundation. (1995). *Kilio Chetu.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Ndimele, O. (1997). *Semantics & The Frontiers of Communication*. Port Harcourt: University of Port Harcourt Press Ltd.

Niculae, V. & Mizil, C. (2014). *Brighter than Gold: Figurative in User Generate Comparisons.* in Proceedings of the 2014 Conference on Empirical Methods in Natural Language Processing, Doha, Qatar, 25-29 Oktoba 2014.

Ragin, C. C. (1987). *The Comperative Method*. Califonia: University of Califonia Press.

Richards, I. A. (1965). *The Philosophy of Rhetoric.* New York: Oxford UniversityPress.

Sacks, S. (ed.). (1979). *On Metaphor.* Chicago: The University of Chicago Press.

Stacy, R. H. (1997). *Defamiliarization in Language and Literature*. New York: Syracuse UP.

Stern, J. (2000). *Metaphor in Context*. Cambridge: MIT Press.

Trick, L. and Kanzi, A. (1986). The Domain Interaction Approach to Metaphor: Relating Individual Differences and Metaphor Characteristics, *Metaphor and Symbolic Activity,* 1(3): 185-213.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3). Nairobi: OUP.

Ullmann, S. (1967). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. London: Oxford Basil Blackwell.

Magazeti: *Majira*, *Mtanzania* na *Mwananchi* yaliyochapishwa tarehe 21/01/2017.